BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

OORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 25 Mei, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii**:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

88. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha Vikosi Maalum hapa Zanzibar vinavyotekeleza vyema majukumu yao ya kikatiba na kisheria. Pamoja na utekelezaji huo, askari wetu wa vikosi hivyo wanakabiliwa na changamoto kadhaa katika utumishi wao ikiwa ni pamoja na kutolipwa ipasavyo fedha zao za likizo pamoja na kuziomba na kupewa likizo pekee.

(a) Je, Serikali ina ufahamu upi wa fedha za likizo zinazostahiki kulipwa kwa askari wetu wa Vikosi pale wanapopewa likizo zao za kisheria.

(b) Je, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ni askari wangapi wa Vikosi vya SMZ wamelipwa pesa zao za likizo.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimelipwa kwa kila askari kwa mwaka 2022/2023 kama ni malipo ya likizo zao kisheria.

89. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni jambo linalofahamika kuwa, askari wetu wa Vikosi vya Idara Maalum kama ilivyo kwa watumishi wa Umma, wana wajibu wa kutumikia utumishi wao sehemu yoyote ya Unguja na Pemba, na inapohitajika kupewa uhamisho huo, wana haki ya kupewa nauli na posho la kuwafikisha katika sehemu zao mpya za kazi.

Kwanini askari hao hawapewi fedha za uhamisho pale wanapopewa uhamisho wa kwenda Pemba au Unguja na badala yake hupewa tiketi na Tsh. 10,000/= tu wakati tukijua kuwa nyumbani wana familia zinazowategemea.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

18. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Miongoni mwa ahadi za Serikali ni kuongeza mapato ya nchi kwa kuimarisha vyanzo vilivyopo na kuibuwa vyanzo vipya vya mapato.

Je, ni vyanzo gani vipya vimeibuliwa hadi sasa.

122. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kuna haja ya kuifanya Wizara yetu yenye dhamana na Fedha kuwa kitovu cha kutunga, kuchunga na kutathmini sera za kodi, fedha na utengenezaji mitaji ya kujenga uchumi nchini. Hata hivyo, miongoni mwa changamoto zinazoikabili Wizara ni pamoja na kukosekana wachambuzi wa kutosha wa mambo ya uchumi na fedha kama ilivyowasilishwa kwenye Bajeti ya 2022/2023.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mfumo bora wa kitaasisi ambao utajenga weledi na uwezo wa kiutendaji.

(b) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba suala la kodi ya mapato linatolewa rasmi katika orodha ya mambo ya Muungano sambamba na mafuta na gesi asilia.

(c) Je, Serikali imeshachukua hatua gani kuelekea kuanzishwa kwa soko la hisa Zanzibar na ni lini mpango huu utakamilika.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

70. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mradi wa ujenzi wa barabara ya Kipapo Mgelema – Wambaa umeanza kwa muda mrefu sasa, lakini bado unasuwasuwa katika ujenzi wake.

(a) Je, kuna sababu zipi zinazopelekea kukwama kwa mradi

huo kwa kipindi cha muda mrefu sasa.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wanaoitumia barabara hiyo.

101. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa nia njema na baada ya kuchelewa kwa miaka mingi, Serikali imeanza ujenzi na uhuishaji wa barabara kongwe ya Chake Chake–Wete. Hata hivyo, malipo ya fidia kwa nyumba za kuishi watu zilizo karibu na barabara hiyo ni madogo sana kulingana na uhalisia wa thamani ya nyumba kwa kipindi cha sasa.

(a) Je, ni utaratibu upi hutumika katika kuvunja nyumba za wananchi ambao bado wanaishi katika nyumba zao.

(b) Je, ni upi msingi wa tathmini ya nyumba zilizovunjwa na zinazoendelea kuvunjwa katika barabara kongwe ya Chake Chake–Wete inayofanyiwa ujenzi mpya.

(c) Je, ni upi wastani wa malipo kwa nyumba moja na wastani wa kusubiri fidia tokea nyumba kuvunjwa.

## <u>Wizara ya Afya:</u>

44. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuandaa huduma shirikishi za afya ya uzazi na watoto. Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la vifo vya watoto wachanga wakati wa kuzaliwa na baada ya kuzaliwa.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kuongezeka kwa vifo hivyo.

(b) Je, vifo hivyo vinatokea kwa wingi kwenye maeneo gani ya nchi yetu.

(c) Katika maeneo yanayotokea vifo hivyo kwa wingi, je idadi ya wafanyakazi wanaotoa huduma ya afya inaridhisha kwa kiasi gani.

113. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyo dhahiri, kumekuwa na tabia iliyozoeleka kwa baadhi ya viongozi na wananchi wengine kutumia viyoyozi (ACs) kulikokithiri bila ya kufuata miongozo yoyote ya kiafya. Jambo ambalo linasababisha kwa kiasi kikubwa maradhi kwa watumiaji hasa kwa vile kunakuwa na tofauti kubwa ya nyuzijoto kati ya mazingira yenye kiyoyozi na yasiyo na kiyoyozi.

(a) Je, Serikali ina muongozo wowote ulio rasmi wa matumizi ya viyoyozi (ACs) ili kupunguza athari zake.

(b) Je, ni ipi tofauti ya nyuzijoto inayoruhusiwa rasmi kiafya katika nchi yetu kati ya sehemu yenye ACs na isiyo na ACs.

(c) Je, kitakwimu, athari gani za kiafya katika nchi yetu zilizosababishwa na mabadiliko ya tabianchi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

78. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika skuli ya Mtangani iliyoko katika jimbo la Kiwani, kuna upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa sekondari, kiasi ya kukosekana hata mwalimu mmoja wa masomo ya hesabu, ‘biology’ na ‘chemistry’.

(a) Je, kwa kiwango gani Mhe. Waziri unalifahamu suala hili.

(b) Je, Wizara yako itachukua hatua gani ili kupunguza tatizo hilo.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

22. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni haki ya kila mwananchi, na kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa katika maeneo mbali mbali ya jimbo la Wawi, kuhusiana na kupatikana huduma hii.

Je, hali hiyo inasababishwa na nini.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2023/2024.

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
25 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA